kutupwa Jehanam. Kila kitendo cha siri kitafichuliwa (1Wakorinto 4:5) na Mungu atamlipa kila mtu sawasawa na matendo yake, hata yakiwa mazuri au mabaya (Yeremia 17:10; 2Wakorinto 5:10).

Je, dhambi zako za siri zaweza kusimama mbele ya mwanga wa utukufu wa Mungu? Sasa, ikiwa mawazo yako yalirekodiwa kwa muda wa mwaka, na baadaye kuonyeshwa kwa ndugu na marafiki zako? Ungefedhehekaje? Haibu ya aina gani utakayopata mbele za Mungu siku ya hukumu? Huwezi kusimama mbele ya Mungu peke yako. Unahitaji kifuniko cha dhambi zako, na kifuniko hicho ni kupitia kutubu mbele za Mungu na kumwamini Yesu Kristo, sababu "hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa watu kuwaokoa" (Matendo 4:12). Yesu Kristo hakuwa nabii tu. Amesema, "Yeyote aliyeniona, amemuona baba" (Yohana 14:9); "Mimi na baba tu mmoja" (Yohana 10:30); "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Hakuna ajaye kwa baba ila kwa mimi" (Yohana 14:6). Tunaweza kuja kwa Mungu na kusamehewa dhambi kupitia Yesu peke yake (Matayo 7:13-14).

Unawaza tu kusamehewa kutoka hasira za Mungu, kwa neema, kwa imani na kupitia Yesu peke yake. Kwa wewe kusamehewa na kupokea karama ya Mungu ya wokovu, unapaswa kutubu; maana yake unapaswa kugeuka kutoka maisha yako ya dhambi na kumgeukia yesu. Unapaswa kukiri kwamba umemtendea Mungu dhambi. Unapaswa kuwa na huzuni ya dhambi zako ajili ya kumkosea Mungu. Unapaswa kuamini kwamba Yesu alikufa msalabani ajili ya dhambi zako. Kutubu ni zaidi ya kumwambia tu Mungu kwamba umejutia. Kutubu kwako kukiwa kwa kweli, ikiwa ni Mungu anayetumika ndani ya roho yako, bila shaka itadumu maisha yako yote. Roho Mtakatifu atakuja kuishi rohoni mwako na kukufanya kiumbe kipya katika Kristo. Dhambi zako zote za zamani, za sasa na zijazo zitafutiliwa mbali milele. Utazaliwa upya kiroho. Utakubaliwa katika familia ya Mungu na hutokuwa tena mtumwa wa dhambi. Utazaa matunda ya toba (Matayo 3:8). Utaanza kupenda vitu vizuri ulivyokuwa ukivichukia, na kuchukia vitu vibaya ulivyokuwa ukivipenda.

Biblia inasema, "Siku ya wokovu ni sasa", unapaswa kutubu na kumwamini Yesu Kristo sasa (2Wakorinto 6:2). Usipoteze muda sababu hujui utakufa lini (Luka 12:20). Mungu anakupa rehema kupitia Yesu, kwa hiyo usifanye moyo wako kuwa mgumu mbele za Mungu (Waebrania 3:8). Omba Mungu usiku kucha ikiwezekana, ili akujalie kuiamini Biblia na kutubu, sababu hii ni karama kutoka Mungu (Waefeso 2:8). Siyo maombi yako ndio itakayokuokoa. Maombi sio kama kutumia kidonge. Fungua roho yako mbele za Mungu, asemaye, "...Lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu" (Isaya 66:2b). Kwa hiyo, fungua roho yako, na uivunje mbele za Mungu. Jinyenyekeze mbele za Mungu na atakuinua (Yakobo 4:10).

Mungu anaamuru kwamba utubu na kuiamini injili ya Yesu. Ukija kwa Yesu kristo kupitia imani yenye kuokoa, chukua Biblia, uisome kila siku na ufuate yote isemayo. Baadaye tafuta kanisa lenye kuhubiri Biblia na uanze kukusanyika na wengine. Shiriki katika ubatizo wa waamini, kama ushuhuda wa maisha yako mapya ndani ya Kristo (Matendo 2:38).

Nini kinachotokea mtu anapofariki?

Nini kinachotokea mtu anapofariki? Je, watu wanaenda mahali pema wanapofariki? Je, wewe utaenda wapi? Watu wengi hufikiri kwamba watu "wazuri" huenda mbinguni na watu "wabaya" huenda jehanamu. Wengi hufikiri kwamba, mtu akitenda mema kuzidi mabaya, huyo ataenda mbinguni. Wamoja huamini kwamba wakiua, wanaweza wakafidia kwa kutenda mema. Wengine huamini kwamba wakifanya kitendo "kibaya", wanaweza kumwomba Mungu msamaha na kumuahidi kutorudia tena kosa hilo na watasamehewa. Unaweza ukajua namna gani kwamba umefanya mema kiasi? Utajuaje kwamba msamaha wako ni mzuri kiasi?

Hebu tutazame ikiwa hii inawaza ikatumika kwenye sheria za kiraia. Mtu fulani aliwaibia na kuwaua watu, na sasa amesimama mbele ya hakimu. Mashahidi waliomuona akifanya uhalifu huo wapo. Kuna kamera iliyorekodi uhalifu wake. Hakimu anamgeukia mhalifu, "Bwana, ushahidi wote upo hapa, una hatia. Una lolote la kusema kabla sijakukatia hukumu?" Mhalifu anajibu, "Ninaamini kwamba wewe ni hakimu mzuri. Naomba samahani kwa mauaji na wizi wangu. Nahisi vibaya na ninaahidi kutorudia makosa hayo mara nyingine. Niache niende, nitakuja nyumbani kwako kumaliza yote. Je, hii inaweza kutumika ikiwa hakimu ni mzuri?

Ikiwa hakimu ni wa haki, anapaswa kufuatilia sheria na kumuadhibu mhalifu. Hakimu angesema, "Mimi ni hakimu mzuri. Ni vizuri kwamba unatubia makosa yako. Jutia na usirudie makosa hayo tena; ila, sababu mimi ni hakimu mzuri, ninapaswa kufuata sheria. Wewe ni muuaji na sheria inaomba uuliwe". Hakimu anapaswa kumwadhibu mhalifu huyo kwa kukeuka sheria. Kitu chochote mhalifu anachompa hakimu, huwa hongo. Hebu tutazame kipimo ambacho kimekuwepo kwa muda wa miaka mingi, "Amri kumi" (Kutoka 20). Hizi ni amri Musa alizopewa na Mungu. Hebu tutazame ikiwa wewe ni mtu mzuri kufuatana na, ikiwa umetimiza mbili kati ya hizi amri.

Amri ya 6 inasema, "Usiue" (Kutoka 20:13). Kweli, hujawahi kumuua mtu awaye yote, ila Yesu alisema, "Ukimchukia ndugu yako bila sababu, uko muuaji" (Matayo 5:22). Yesu alisema, ukimlaani jirani yako au ukikataa kumsamehe, unastahili hukumu. Je, umewahi kumchukia mtu, umewahi kukataa kusamehe mtu, au umewahi kumlaani mtu yeyote? Ikiwa umewahi, Biblia inasema kwamba, Mungu anakuona kama muuaji rohoni (1Yohana 4:20). Wauaji hawataingia mbinguni.

Amri ya 7 inasema, "Usizini" (Ktoka 20:14). Watu wengi ni waaminifu kwa waume/wake wao. Lakini Yesu alisema, "Mtu akimtazama mwanamke na kumtamani, ameishazini naye moyoni mwake" (Matayo 5:28). Je, umewahi kumtamani mtu yeyote? Ungemuonaje mtu mwenye hisia mbaya kwa mume/muke au binti yako? Nadhani ungemuita mpotovu. Ungeona hasira na karaha. Hivyo ndivyo Mungu anavyohisi kwa mtu mwenye tamaa mbaya. Ikiwa umewahi kufanya hivyo, ina maana Mungu anakuona kama mwenye kuzini moyoni. Pengine unasema, "Hii hainihusu, sababu mimi sijaoa". Kufuatana na Biblia, uzinzi wa moyo ni pamoja na uasherati na mawazo mabaya (1Timoteo 1:10). Biblia inasema kwamba, "Mungu atawahukumu wazinzi na washerati" (Waebrania 13:4); na kwamba, watu kama hao hawataingia mbinguni (1Wakorinto 6:9).

Je, uliupita mtihani? Ulivunja mojawapo ya amri hizo? Kuna amri nyingine 8. Biblia inasema, "Uvunjapo sheria moja, utakuwa umevunja yote" (Yakobo 2:10). Muuaji akiwa jela huku anawagawia watu chakula chake, atakuwa amefanya kitendo kizuri, ila atakuwa bado ni muuaji. Mtu anawezakuwa mzuri kuzidi wengine wote, ila kutokana na amri kumi anahukumiwa mbele za Mungu. Biblia inasema, "Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23).

Mungu hakuoni kama mtu mzuri; bali anakuona kwa kipimo chake mwenyewe. Mungu anakuona kama muuaji mwongo.

Je, muuaji mwongo aweza kuingia mbinguni? Je, muda waweza kusamehe dhambi? Ikiwa mtu aliua miaka 30 iliyopita, yeye bado ni muuwaji. Je, unaweza kumlipa Mungu fidia?

Ufikapo nyumbani na kumkuta mtu amewauwa watu wa familia yako, na baadaye akupe dola 10; waweza kumuacha aende zake? Huyo mtu ni mhalifu na anastahili kuhukumiwa. "Ni wewe" ndivyo nabii Nathan alivyomwambia mfalme Daudi baada ya kitendo chake cha mauaji na uzinifu (2Samuel 12:7). Kufuatana na wema wako, huna tumaini la kusamehewa na Mungu. Hata ukijutia, sheria inadai kifo chako. Mungu ni mtakatifu na anaomba ukamilifu wa mawazo, maneno, na matendo. Dhambi yako inapinga utakatifu wa Mungu usio na mwisho; kwa hiyo, adhabu pekee inayostahili dhambi yako ni mateso ya milele Jehanam. Biblia huzungumzia Jehanam kama mahali penye moto, kiza, na kilio. Ikiwa unahitaji kulipia dhambi yako ili kuridhisha hasira za Mungu, ina maana unapaswa kwenda Jehanam milele. Kitu chochote chini ya hicho ni kitendo cha kutaka kumpa Mungu rushwa (Zaburi 49:7-9).

Hebu tazama mfano huu: mtu fulani iliiba Benkini, baadaye kashikwa na kusimama mbele ya hakimu aliyesema, "Una hatia; kwa hiyo lipa dola 1,000,000 au aliyesema, "Una hatia; kwa hiyo lipa dola 1,000,000 au utafungwa maisha". Huyo mtu hakuwa na hela na hakuwa anamjua mtu yeyote ambaye angeweza kumlipia. Maramoja hakimu kaamuru achukuliwe jela. Baadaye, mtu mwingine, ambaye huyo mhalifu hakuwa anamjua, kajitokeza mahakamani na kumwambia hakimu, "Benki huyu mhalifu alimoiba ni yangu. Kwa hiyo, nitamlipia huyu fidia. Hanijui, lakini nimeamua kumuonea huruma hata kama haistahili". Huyo mgeni akalipa deni, baadaye hakimu akamwambia yule mhalifu, "Fidia imelipwa na sheria imeridhishwa. Kwa hiyo, sheria haiombi adhabu yako tena. Uko huru kwenda zako". Je, ungejihisije kuhusu huyo mgeni? Kitendo kama hicho ndicho Yesu Kristo alichokufanyia. Hii ndio habari njema ya Biblia. Ulikua na deni ya dhambi zako ambazo usingaliweza kulipia. Shida sio kwamba umetenda dhambi mara nyingi. Ukweli ni kwamba, hujawahi kufanya kitu chochote kibaya, ila una dhambi mbele za Mungu.

Yesu alijitoa kama kafara msalabani ajili ya dhambi zako (1Petro 3:18). Hakustahili kufa ajili yako, ila aliamua kufa ajili ya upendo na rehema zake. Hasira za Mungu ajili ya dhambi zako zilimuangukia Yesu. Biblia inamwita Yesu, "Mwanakondoo wa Mungu" (Yohana 1:36). Hii ni kwa sababu, wakati wa Musa watu walikuwa wakitoa mwanakondoo ajili ya dhambi (Kutoka 12:3). Hii ni picha ya Yesu, sababu Yesu alijitoa msalabani, akabeba hasira za Mungu ajili ya dhambi zako na akafa kifo ulichostahili kufa. Baadaye akazikwa kaburini na baada ya siku tatu, akafufuka kutoka wafu. Kwa kufanya hivyo, Mungu alihakikisha kwamba deni ya dhambi ilikuwa imelipwa. Msalabani Yesu alisema, "Yote imekwisha" (Yohana 19:30).

Ajili ya kitendo cha Yesu msalabani, Mungu yuko huru kukutangaza kama asiye na hatia. Sheria haina tena uwezo juu yako. Hii ni njia pekee Mungu mwenye haki hutumia kwa kuwasamehe wenye dhambi na wenye hatia, bila kukiuka haki yake timilifu. Hakuna hata mtu mmoja anayestahili kusamehewa. Mungu hutoa zawadi hii kwa neema (Waefeso 2:8). Hakuna kazi au juhudi za kidini unazoweza kutenda ili ustahili zawadi hii. Mungu hakupaswa kukuokoa, bali aliamua kupenda dunia na kuokoa wale ambao watatubu na kumwamini Yesu. Mungu "anaamuru watu wote mahali popote watubu" (Matendo ya Mitume 17:30) na kuamini Injili" (Marko 1:15). Kuamini ni zaidi ya kukubali tu kwamba huu ni ukweli. Unapaswa kutumikia hii imani. Kama ungehitajika kuruka kutoka kwenye ndege, kutia imani kwenye mwavuli (au parachuti) peke yake kusingekusaidia. Unapaswa kufungua mwavuli na baadaye kuamini kwamba mwavuli unaweza kuokoa maisha yako. Kuokoka unapaswa kumwamini Yesu peke yake. Mungu ameandaa siku ambapo atahukumu dunia. Dhambi na kila mwasi atahukumiwa na